

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu: 026 2324343/2324384
Nukushi:0262320046/2320121
Barua pepe : ras@dodoma.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 914
Dodoma



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais mstaafu wa Ireland Mheshimiwa Mary Robinson na Mama Graca Machel ambaye ni Mke wa Rais Mstaafu wa Afrika Kusini Hayati Nelson Mandela, kesho Julai 13, 2017 wanatarajiwa kufanya ziara ya siku moja Mkoani Dodoma.

Wakiwa Mkoani Dodoma viongozi hao watatembelea Zahanati ya kijiji cha Mpamantwa kwenye Wilaya ya Bahi. Aidha, watakutana na kufanya mazungumzo na baadhi ya viongozi wa Serikali akiwemo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Ndugai (Mb.) na Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummu Mwalimu (Mb).

Viongozi hao wastaafu ni wawakilishi wa taasisi ya "The Elders" ya Uingereza iliyoanzishwa na Hayati Nelson Mandela ikiwa na lengo la kushughulikia masuala ya Amani, Haki za Binadamu na Huduma za Afya ambayo kwa sasa ipo chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa Ndugu Kofi Annan .

Baadhi ya wajumbe wake ni viongozi mashuhuri wa nchi mbalimbali duniani waliostaafu wakiwemo Rais mstaafu wa Ireland Mheshimiwa Mary Robinson, Mama Graca Machel na Rais Mstaafu wa Marekani Mheshimiwa Jimmy Carter.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Jeremia Mwakyoma'.

Jeremia Mwakyoma
AFISA HABARI NA UHUSIANO
OFISI YA MKUU WA MKOA DODOMA
Julai 12, 2017